



## **Oman kushiriki sensa ya samaki**

**Dar es Salaam.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ame-sema utafiti utakaofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tafiri) na Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman (OIA), utasaidia kujua idadi halisi ya samaki waliopo Bahari ya Hindi.

Ndaki alisema Serikali iki-jua kiwango hicho italisaid-ia Taifa kuweka mipango ya uhakika katika sekta ya uvuvi.

"Hatujawahi kufanya utafiti tangu tupate uhuru, kwani Inahitaji gharama na teknolojia ya hali ya juu. Kazi hii italeti tija kwa nchi na kwa mwananchi mmoja mmoja kupata maendeleo. Tunaishukuru Serikali ya Oman kufanya kazi hii kwa mwaka mmoja," alisema.  
**(Bakari Klango)**